Nchini Tanzania, Umiliki wetu wa asilimia 20 ya hisa katika Tanzania Breweries umekuwa wenye manufaa na umaarufu wa pombe yetu muhimu Tusker umeongezeka hata kudhibiti asilimia 12 ya soko la nchi hiyo.

Kuhimiza Uwajibikaji

Kadri umaarufu wa pombe zetu unavyozidi kuongezeka katika eneo la Afrika mashariki, ndivyo kujitolea kwetu kunavyozidi katika kuhakikisha kwamba bidhaa zetu zinafurahiwa kwa uwajibikaji. Mnamo mwaka 2006, tulitenga Ksh 125 millioni ili kuhamasisha unywaji wenye kuwajibika. Mbinu zetu zimewafikia wadau wa tabaka mbali mbali wakiwemo wahudumu wa Baa,

Mwanachama wa kundi la E-green apanda miti.

wanaohusika na mapambo na matangazo ya biashara, na umma kwa jumla. Pia tumeandaa warsha na mikakati ya kuzuia watu walio na umri mdogo kunywa pombe miongoni mwa shughuli nyingine.

Njia moja muhimu zaidi ambapo tunaweza kuchangia burudani kamili ya bidhaa zetu kwa uwajibikaji ni kwa kushirikiana na maafisa wa serikali na wahusika wengine katika utungaji wa sera ya taifa juu ya pombe. Matunda ya juhudi zetu nchini Kenya na Uganda yameanza kuonekana.

Miradi ya Jamii

Uwekezaji katika jamii tunakoendesha shughuli zetu ni miongoni mwa mikakati yetu muhimu. Kupitia Wakfu wa EABL, tuliboresha maisha ya takribani watu 250,000 katika Afrika mashariki mwaka uliopita. Miradi kama ule wa Maji kwa uzima ilisaidia kukarabati visima na kutoa maji safi kwa maelfu ya wenyeji wa Afrika mashariki, Ilhali kundi letu la E-Green limesaidia kupanda maelfu ya miti ili kusaidia kutunza mazingira. Pia kupitia kwa mpango wetu wa misaada ya masomo, tumeendelea kuwapa ushauri na misaada wanafunzi wenye mahitaji wakiwemo wanafunzi 20 kutoka Kenya, Uganda na Tanzania mnamo kipindi cha sasa cha matumizi ya pesa.

Nchini Tanzania tunajenga kituo cha matibabu ya kasoro za mifupa huko Arusha. Kwa kushirikiana na Diageo tutazindua mradi mkubwa wa tangi la maji nchini Tanzania ili kufaidi zaidi ya watu elfu-20.

Kampeini ya 'WE ID' yazinduliwa. Kushoto kuelekea kulia: Eric Kiraithe - Msemaji wa Polisi, Ken Kariuki - Naibu Mwenyekiti Nabak, James Waweru - Mkuu wa Mkoa wa Nairobi, Francis Munyororo - Katibu PERAK.

EAST AFRICAN BREWERIES LIMITED

Mwaka wa Mafanikio

Wakfu wa EABL wasaidia jamii kuchimba kisima.

Umaarufu wetu wa ushindani

Tunachojivunia zaidi katika biashara ni wafanyikazi wetu wenye ujuzi. Wafanyikazi wetu na wengineo wenye bidii ambao hujihusisha na wasambazaji na pia wauzaji wa bidhaa zetu wametufanya kuwa kampuni inayopendelewa na wengi katika eneo zima la Afrika mashariki. Mnamo mwaka uliopita, tumefanya kila juhudi kuwaunga mkono watu hao kupitia mipango mipya inayosisitiza fikira za mafanikio na kuhimiza uongozi na pia kubuni utaratibu wa umoja wa makundi ili kuendesha shughuli zetu kama kampuni moja. Vishawishi kama vile mtindo wa malipo yanayotegemea bidii ya mtu vinatambua matokeo ya utendaji kazi miongoni mwa wafanyikazi wetu walio na bidii zaidi. Vile vile tunaendelea kuzingatia maadili mema na wafanyikazi wote kudumisha sifa nzuri ya kampuni.

Mgao wa Faida

Bodi inafuraha kupendekeza mgao wa faida wa mwisho wa Ksh 5.55 kwa kila hisa ambao pamoja na mgao wa muda wa Ksh 2.15 kwa kila hisa uliolipwa mwezi April 2007 unafanya mgao wote wa faida kwa mwaka huo kuwa Ksh 7.70. Hii inawakilisha ongezeko la 34% ikilinganishwa na mgao wa faida wa mwaka uliopita. Malipo kwa hisa yaliongezeka kwa aslimia 14%.

Ushuru

Katika kipindi cha mwaka huo kampuni ililipa jumla ya Ksh 3.1 bilioni ambalo ni ongezeko la Ksh 940 milioni kutoka mwaka jana katika ushuru wa moja kwa moja na usio wa moja kwa moja kwa hazina kuu za Kenya, Uganda na Tanzania na bila shaka kuifanya kuwa kampuni inayotoa ushuru mkubwa zaidi katika eneo hili.

Matarajio

Kulingana na matarajio yetu ya siku za usoni, tumejitolea kujenga kundi moja imara katika shughuli zetu, kote katika eneo la Afrika mashariki. Kwa kuweka katika watu wetu, bidhaa maarufu na mbinu za uuzaji, teknolojia mpya na miradi yenye manufaa kwa jamii, tunapanga kuboresha sifa ya EABL kutoka ngazi ya kampuni inayopendelewa na wengi katika Afrika mashariki hadi ngazi za kimataifa. Hatua yetu ya uwekezaji mkubwa katika shughuli muhimu ya marekebisho kwa kutumia taratibu,mbinu na maarifa ya tarakilishi(SAP) imetuwezesha kuzindua mpango wa kuimarisha utendaji kazi na pia ustadi wa kupanga.

Utekelezaji wa marekebisho ya SAP utabadili jinsi watu wanavyofanya kazi na kulainisha kampuni yetu. Habari zitakuwa bayana zaidi na pia kupatikana kwake kutakuwa rahisi na hivyo kuifanya kampuni hii kutekeleza majukumu yake kwa njia ifaayo zaidi. Wafanyikazi wote wa uuzaji sasa wana vifaa vya Blackberry wireless ambavyo vinawapa fursa ya kuwasiliana kila mara na wenzao wanaohusika pia na shughuli ya uuzaji. EABL imewekeza pia kiasi kikubwa cha pesa katika vifaa vya mawasiliano ya IP ambavyo vimeundwa hasusan kuimarisha utendaji kazi na ubadilishanaji habari haraka na kwa gharama ya chini zaidi.

Washirika

Juhudi zetu za kukua na kuimarika kama kampuni hazingeweza kupata mafanikio yanayohitajika bila uongozi bora wa bodi ya wakurugenzi, na pia zaidi ya wafanyikazi wetu 1,000. Wateja wetu, wauzaji wa reja reja,wauzaji wa jumla, na wagawaji wengine wa ki-biashara pia wanahitaji kupongezwa kwa bidii na imani yao. Tunatumai kuzidisha matarajio ya mwaka 2008 huku tukitatazamia ukuaji wa faida yetu na mafanikio mema mwaka ujao.

J. Kierieni
Mwenyekiti

G. Mahinda
Mkurugenzi Mkuu

Rasilimali yenye umuhimu zaidi

Maafisa wetu wanaendelea kutoa ushindani wa hali ya juu kibiashara kwa kukuza na kuunganisha talanta za kibinafsi na kisha kushirikisha talanta hizo kwa kubuni "mbinu mwafaka za malengo ya ukuaji". Kwa njia hiyo wafanyikazi wetu wanaonewa kijicho na kampuni nyingine za humu nchini na pia kanda hii. Kwa kuboresha uwezo wa kila mfanyikazi na kuhimiza hisia nzuri na zenye maendeleo, tumejipatia heshima ya "mwajiri anayestahiki" katika kanda hii. Pia tunatambua kwamba maeneo mbali mbali ndiyo chanzo cha maarifa na ujuzi ambavyo vimejaribiwa katika chumi zilizostawi na vinaweza kufanikisha huduma za kampuni yetu nchini Kenya na Uganda hadi viwango vya kimataifa. Hii ni kuambatana na lengo letu la ukuaji na kuhusishwa kwa wote.

Kampuni moja, Desturi Moja

Tunachukulia umoja wa mpangilio wa shughuli zetu kuwa mali na hatua yenye umuhimu mkubwa kwa mipango yetu ya ngazi za juu. Tunatilia mkazo desturi ya umoja wa wafanyikazi kwa kuwianisha taratibu, kuelekeza pamoja taratibu hizo hasa nyoyo na fikira za wafanyikazi katika njia moja ya kufanya kazi, kutimiza lengo moja. Pia tumeboresha mawasiliano kati ya wafanyikazi na wasimamizi katika juhudi za kukuza ushirikiano wa ki-kazi.

Tunaamini kwamba kuwapa wafanyikazi uwezo wa kisaikolojia Kuambatana na maongozi yetu ya "'msimamo"' kutaendelea kutuwezesha kutimiza malengo yetu:

Sote ni kitu kimoja.
Twawezesha na kuongoza kwa vitendo.
Tunaheshimu azma yetu ya kuafikia matokeo ya kipekee.

Wafanyikazi washiriki kwenye zoezi la kuimarisha ushirikiano.

Kukuza Viongozi

Mtindo wa uongozi wetu kibiashara umechangia sana ufanisi wa kampuni hii kwa kipindi cha mwaka uliopita. Tulitambua uongozi wa ushawishi kuwa mbinu moja muhimu, tukafafanua kwa pamoja maana ya uongozi na tukajifunza kutambua uwezo wetu na vipaji katika fani hii. Tulianzisha mtindo wa fikira za mafanikio miongoni mwa wasimamizi wetu ili kuboresha azma, umiliki wa mbinu na kutegemeana. Hatua hiyo kwa upande wake, imeongeza kasi ya utekelezaji wa shughuli zetu mbali mbali, Ubora wa juhudi zetu na mtindo wa kutegemea wa kuafikia matokeo. Tungali katika hatua za mwanzo za barabara hii ya "fikira za mafanikio lakini tunatumai kwamba tutakuwa na mafanikio mema zaidi mwaka ujao.

Taratibu mpya, Mafanikio zaidi

Tunaendelea kulenga ustadi wa taratibu zetu ili kudumisha zile zinazoweza kusaidia mbinu zetu kibiashara na pia kuvutia na kudumisha watu katika ujuzi ufaao. Kuambatana na hali hii, tumetekeleza utaratibu maalum wa marekebisho SAP (katika idara zote za kibiashara isipokuwa East African Maltings Limited) katika mwaka uliopita wa matumizi ya pesa, hali itakayoboresha zaidi hali ya utendaji kazi Kwa kukuza na kudumisha taratibu hadi njia rahisi za kutayarisha maagizo ya mauzo na upatikanaji wa pesa za mauzo hayo, kuweka rekodi bora za kumbukumbu na kutoa habari kuhusu shughuli za kibiashara sawia na kuwianisha shughuli nyinginezo.

Kuwekeza katika watu wetu

Kundi la Masuala ya Wafanyikazi katika siku yao ya mapumziko ya mwaka.

Utaratibu huo wa marekebisho SAP pia umeleta desturi mpya miongoni mwa watumiaji wa mwisho huku kukiwa na nidhamu ya hali ya juu na msimamo fulani ukizingatiwa katika kila hatua. Pia tumelenga usimamizi unaoleta faida ya jumla ki-biashara ili kuweza kuchunguzwa na kudhibitiwa kwa karibu, tofauti kuondolewa na mikakati ya uimarishaji wa mara kwa mara kuwekwa.

Vishawishi-Vya Ukuaji

Pia tumeratibu vishawishi vya aina zote za biashara zinazohitajika kwa kila kundi ili kusaidia katika kuafikiwa kwa malengo. Hayo pamoja na taratibu za malipo zinazoambatana na bidii za maajenti wetu wa uuzaji (Mtindo ulioanzishwa majuzi nchini Uganda ili kwenda sambamba na ule wa Kenya) yameboresha mtizamo wetu wa makadirio ya utendaji kazi na kutimizwa kwa malengo ya kila siku, kila wiki na kila mwezi. Ili kudumisha wafanyikazi wenye ujuzi sera zetu za malipo zimeendelea kuambatanishwa na ufanisi wa biashara na bidii ya wafanyikazi binafsi.

Kuthamini wengine

Tunaamini kwamba mafanikio ya biashara yanategemea jinsi tunavyotangamana, kusaidiana na kuheshimiana na juu ya yote jinsi tunavyothamini wenzetu. Hapo ndipo maadili mema yanatambuliwa kuwa msingi wa shughuli zetu huku tukidumisha sifa bora ya kampuni katika ngazi zote za biashara. Maadili hayo ni pamoja na kuto-vumiliwa kwa tabia yoyote ambayo haiambatani na matarajio ya kampuni.

Masomo kwa mtandao

Pia tumejitolea kuendelea na uwekezaji katika wafanyikazi wetu, Mimea na taratibu mbali mbali za mipango ya masomo kwa njia ya mtandao, ambayo inalenga uongozi wa kibiashara na masomo mengineyo. Wafanyikazi wetu sasa wanaweza kusoma kwa usaidizi wa vifaa vya kimataifa ikiwa ni pamoja na huduma za maktaba za shule ya kibiashara ya Harvard. Kuweko kwa huduma za internet za kampuni kunawezesha wafanyiakazi wetu kukua na kusoma kuambatana na uwezo wao wenyewe.

Hakikisho la Ubora

Tunaendelea kutumia kimea bora zaidi katika utayarishaji wa pombe zetu katika eneo la Afrika Mashariki.

Tumeweka mfumo madhubuti wa hali ya juu, kuanzia kwa mali ghafi hadi katika kiwanda cha upakiaji na kwenye soko.

Utaratibu huu unasaidiwa na mfumo bora tulioweka kama ilivyothibitishwa na cheti cha shirika la ukadiriaji ubora wa bidhaa nchini, ISO, EMS-Mfumo wa usimamizi wa mazingira, mifumo ya usalama kazini na afya OHSAS. Mifumo yetu yote hukaguliwa mara kwa mara kindani na kupitia wataalamu kutoka nje.Tuna mfumo madhubuti wa kupokea maelezo na maoni kutoka kwa wateja ambao ripoti yake huzingatiwa kila mara katika kuchambua kiini ili kuimarisha mifumo na taratibu zetu.

Chombo cha huduma mara mbili katika kiwanda cha EABL-Uganda.

Katika biashara yetu ya gilasi tunaendelea kuwekeza katika usimamizi bora na tulitunukiwa ISO 9001 2000, EMS 14001 2004 na cheti kingine cha HACCP pamoja na OHS 18001 1999. Vyeti hivi vinadhihirishia wateja wetu kwamba tunaendesha kiwanda cha kiwango cha kimataifa cha gilasi.

Nchini Uganda mifumo yetu ya usimamizi bora imesaidia kujenga msingi thabiti kwa biashara yetu ya kiwango cha kimataifa ambayo tunajitahidi kila mara kuiimarisha. Wakati wa mwaka huo mifumo yetu ilifanyiwa ukaguzi na wataalamu kutoka nje na kuifanya kupata tuzo zinazotambuliwa kimataifa ikiwa ni pamoja na ISO 9001:2004 na cheti cha HACCP, cheti cha uhifadhi mazingira ISO 14001:2004 na utambuzi wa UNBS.

Katika shughuli zetu zote tunaendesha biashara kwa njia inayowajibikia mazingira kulinda na kuimarisha hali ya watu wetu, bidhaa na jamii ambako tunafanya kazi na kuishi. Ili kuafikia lengo hili tumejitolea kusaidia udumishaji na uhifadhi mazingira kupitia uimarishaji wa mara kwa mara na uzuiaji, uchafuzi kama ilivyodhihirishwa na uwekezaji wetu wa juu katika kiwanda cha kisasa cha usafishaji maji taka.

Ufanisi katika kudhibiti gharama

Kiwango cha gharama ya uzalishaji bidhaa za kuuzwa kwa kila hektolita kilipungua kwa 21% licha ya shimkizo za kupanda kwa gharama ya maisha. Kujitolea kwetu kudhibiti gharama kumeendelea kuwa thabiti na tunatarajia kupunguza kwa kiwango cha 27% zaidi gharama ya bidhaa zinazouzwa kwa kila hektolita kufikia mwisho wa mwaka huu wa matumizi ya fedha.

Uuzaji,Uvumbuzi na Maendeleo

Ili kuafikia malengo yetu mwaka huu ajenda yetu ya uuzaji ilizingatia maeneo matatu kwa uimarishaji yanayohusisha kuzingatia upya wateja, mipango ya kuelekea sokoni na shughuli za kuimarisha aina maarufu za bidhaa.

Sisitizo Juu ya Wateja

Wakati wa kipindi cha mwaka huo, tulifanyia marekebisho muundo wetu wote wa uuzaji ili kusisitiza zaidi juu ya wateja wetu. Tuliongeza idadi ya wafanyikazi wa uuzaji nyanjani maradufu na kuimarisha huduma nyinginezo za kuendeleza shughuli za uuzaji. Manufaa ya kuimarika kwa huduma kwa wateja wetu na huduma nyingine yanadhihirishwa wazi na ukuaji katika mauzo.

Mipango ya Kuelekea Sokoni

Tuliendelea kutekeleza mradi wa rejareja unaozingatia kuboresha mfumo wa kuelekea sokoni, ugawaji na kuimarisha uwezo. Mpango huo unaofahamika kama 'Project Sambaza', unahusisha mfumo wa kifedha unaolenga wagawaji wetu kwa ushirikiano na benki moja ya humu nchini. Utekelezaji wa marekebisho ya SAP pia umesaidia pakubwa katika kuimarisha utoaji huduma. Tukiendelea mbele, hivi karibuni tutazindua shule ya Tusker Academy ili kuboresha zaidi uwezo wa uuzaji na usambazaji wetu.

Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni Gerald Mahinda pamoja na wafanyikazi wa Diageo na jamii ya Kenya huko Diageo. Wafanyikazi wa makao makuu kwenye uzinduzi wa Tusker huko Uingereza.

'Tunajitahidi kuendeleza sisitizo letu kwa wateja hadi ngazi nyingine kwa kutoa tajriba ya hali ya juu kwa burudani yenye uwajibikaji.'

Shughuli za kukuza aina za bidhaa

Tulijitahidi pia kuimarisha utekelezaji wa shughuli za uuzaji wa aina maarufu zaidi za pombe, Tusker, Guinness na Richot. Ufanisi wetu ulitokana na uwezo wa hali ya juu wa utekelezaji na utekelezaji shughuli kwa wakati ufaao. Mwaka huo ulijumuisha kuimarishwa kwa shughuli za uuzaji zilizodhamiriwa kujenga upya aina maarufu za bidhaa zetu ili kwenda sambamba na ushindani uliopo.

Haswa tuliwekeza katika mipango mipya kama vile mchezo wa televisheni wa Tusker Project Fame ambao ulikuwa wa

Siku za awali: Lori la EABL katika shughuli ya usambazaji bidhaa.



Malori ya usambazaji bidhaa sasa yameimarishwa kwa utekelezaji bora.

kwanza wa aina yake na ambao ulihisisha wanamuziki wa Afrika Mashariki. Mchezo huo ulifurahiwa sana kwenye soko. Pia tulizindua pombe aina ya Tusker Sports ambayo ilitusaidia katika uhamasishaji wakati wa makala ya 35 ya mbio za nyikani za IAAF zilizofanywa Mombasa ambapo tulishiriki katika udhamini wake. Shughuli nyingine za michezo ya Tusker ni pamoja na mashindano ya Golf na Rugby.

Guinness ilizindua kampeini yake ya 'Greatness' yaani umaarufu, ambayo iliboresha zaidi umuhimu wa pombe hii kwa wateja kama ilivyodhihirika kwa mauzo ya juu katika kipindi hicho cha mwaka. Pia tulitafuta njia mpya za kuendeleza ubora wa maarifa ya wateja wa pato la chini kwa kuhamasisha aina ya pombe ya Senator keg.

Hatimaye tuliboresha kitengo cha mvinyo kwa kuanzisha tena mvinyo wa VAT 69 Scotch whisky kwenye soko. Uzinduzi huo pamoja na matangazo ya kwanza ya kibiashara kuhusu mvinyo aina ya Richot na shughuli zilizohusisha Johnnie Walker, Smirnoff na Baileys, ulisaidia kuafikia malengo yetu kwa kitengo hiki.



Msisitizo Uganda

Nchini Uganda, tuliimarisha mauzo pamoja na uhusiano na wateja wetu. Kundi letu la uuzaji la Bell Lager lilizindua moja ya awamu mbili za kampeini ya ubora kuwasilisha thamani ya aina hii ya mvinyo kama vile ladha nzuri na umbo la kupendeza. Bell Lager pia inawafikia wateja kupitia udhamini wa muziki ikiwa ni pamoja na tuzo za Pearl of Africa Music Awards. Kundi la Senator Lager liliandaa tamasha mbalimbali za kitamaduni kwa lengo la kuwavutia wateja wake muhimu.

Mvinyo wa Uganda waragi sasa unauzwa kwa chupa za 100ml na 200ml na unaendelea kutia fora. Kampeini kwa jina 'The spirit that binds us' 'Mvinyo unaotuunganisha" ilianzishwa katika kipindi cha mwaka huo ili kuimarisha maoni ya wateja wa pombe ya Uganda Waragi. Pombe ya Guinness pia ilianzisha kampeini ya umaarufu, "Greatness" nchini Uganda. Pombe hiyo mwanzo ilihusisha wafanyikazi katika juhudi zake za uhamasishaji na kisha kuzindua kampeini zilizolenga wafanyibiashara na wateja. Kundi la Guinness pia lilidhamini mashindano ya mchezo wa Rugby kufuatia kuongezeka kwa umaarufu wa mchezo huo nchini Uganda.

EAST
AFRICAN
BREWERIES
LIMITED

Kuimarisha taratibu za kindani

SAP zaleta matokeo

Uwekezaji

East Africa Breweries imekamilisha kwa ufanisi mpango wa kuimarisha uwezo wa utendaji kazi na upangaji kwa kuimarisha tekinolojia yake kwa kutumia taratibu, mbinu na maarifa ya tekinolojia (SAP).

Tumewekeza takriban Ksh bilioni moja kutekeleza mpango madhubuti zaidi wa SAP katika Afrika Mashariki.

Tekinolojia hii inawezesha kampuni kutathmini habari zake zinazonakiliwa katika shughuli za kila siku pamoja na habari nyinginezo za hapa na pale kutoka pembe zote za kampuni kusaidia kuchukua hatua za haraka kuhusiana na mabadiliko ya soko. Tekinolojia pia ina uwezo wa kushirikisha shughuli zote za kampuni na kufanya uenezaji habari kuwa rahisi na wa haraka

Mapato

Utekelezaji wake umefanya kazi kuimarisha utendaji kazi na kupunguza gharama ya uendeshaji inayopatikana pale tekinolojia tofauti za tarakilishi zinapotumiwa katika idara mbalimbali za biashara, kuimarisha utendaji kazi kote katika kampuni.

Matawi yetu ya utengenezaji, uchungaji, kimea na utengenezaji gilasi yatatumia tekinolojia hii mwaka huu kuwianisha vipengee vyote vya uendeshaji kutoka kiwango cha utengenezaji hadi usafirishaji bidhaa.

Ufanisi wa tekinolojia ya SAP hauimarishi tu jinsi tunavyofanya kazi bali pia jinsi tunavyoweza kuwasilisha bidhaa zetu kwa haraka sokoni.Kupatikana kwa vyanzo bora vya takwimu kwa haraka kunatuwezesha kujua zaidi kuhusu utendaji kazi wa biashara yetu na muhimu pale ambapo tunahitaji kufanyia marekebisho au kuimarisha

Utekelezaji wa SAP umebadilisha jinsi watu wetu wanavyofanya kazi na kuifanya kampuni yetu kutekeleza kazi yake kwa njia bora.

Kenya

Biashara ya pombe ilikua kwa aslimia 30% wakati wa mwaka huu, ambao ni ufanisi mkubwa. Ukuaji huo ulichochewa hasa na biashara ya pombe za Tusker, Guinness na Senator Keg.

Tuliimarisha shughuli ya upakiaji kwa kuongeza uwezo wake kwa kuweka laini mpya kutoka kiwanda chetu cha Kisumu kwa muda mfupi kwa gharama ya chini ya Kshs. 275 milioni. Uwekezaji huu ulituwezesha kuboresha sana uwezo wa pombe zetu za chupa kwa kiasi kikubwa wakati tulipokabiliwa na changamoto za ugawaji kwa mfano wakati wa msimu wa Disemba mwaka 2006. Kwa sababu hiyo shughuli nchini Kenya na Uganda ziliuza kiwango kikubwa zaidi kuwahi kuuzwa mnamo mwezi Disemba - rekodi ambayo EABL ilikuwa haijawahi kufikia.

Kuwekeza Kshs. 35 milioni kwa kuweka laini ya nne ya kutia pombe kwa chupa kulituwezesha kuongeza uwezo wa pombe ya Keg kwa aslimia 30%. Kadhalika tulizindua mipango ya kuongeza uwezo wa kutengeneza, kugandisha na kuchunga kuanzia mwezi Mei 2007. Pia tuliwekeza Kshs. 900 milioni katika chombo cha kuchunga machicha, kifaa kingine cha kuchunga machicha, vyombo viwili vya huduma mara mbili vya lita 400,000 kila kimoja na mifereji ya kisasa ya kuchunga pombe. Uwekezaji huu utaimarisha uzalishaji, kupunguza uharibifu, kupunguza gharama, na kuongeza ubora wa bidhaa zetu.

Biashara ya gilasi ilinawiri mara dufu kwa ukuaji wa aslimia 130 ikilinganishwa na



Chombo cha utekelezaji huduma mara mbili kinawasilishwa katika kiwanda cha EABL-Kenya.

mwaka uliotangulia, huku gilasi zote zikinunuliwa na wateja wetu. Kwa mara ya kwanza katika historia ya biashara yetu, tuliuza zaidi ya tani 35,000, ambazo zinawakilisha utumiaji kikamilifu wa tanuu zetu. Tunaendelea kuuza bidhaa zetu kwa soko zima la Afrika Mashariki na hivi majuzi tumeenea hadi Malawi, Angola na Namibia.

Uzalishaji wetu wa shayiri mnamo mwaka huo ulifikia tani 90,000, zikidhihirisha ukuaji wa aslimia 24% katika mahitaji. Kiwango cha tani 4,632 za mbegu za shayiri ziliwasilishwa na zinatayarishwa kwa upanzi katika msimu wa sasa na mpango wetu wa uimarishaji shayiri umetoa aina nyingine nne ambazo zilitolewa na Taasisi ya Afya ya Mimea nchini. Kadhalika tulifanya kandarasi na Lesiolo Grain Handlers, watayarishaji wa kisasa wa nafaka kushughulikia utayarishaji wa shayiri yote kavu kabla haijatengenezwa. Lesiolo Grain Handlers wanahakikisha kwamba shayiri yetu inatayarishwa kwa wakati ufaao na kwamba ni bidhaa ya hali ya juu pekee inayosafirishwa hadi Nairobi.

Uwekezaji wa mtaji wa Kshs.150 milioni umeimarisha uzalishaji na ubora wa kimea katika kiwanda chetu kilichoko Kampala Road, jijini Nairobi. Uwekezaji wetu ulijumuisha mtambo mpya wa barafu, ukarabati wa vyombo vya usafirishaji na kuwekwa kwa tangi lingine la maji moto. Kutokana na uwekezaji huo, kiwango cha utoaji kimea kiliongezeka kutoka wastani wa 79 mwaka uliopita hadi 83 mwaka huo. Kadhalika utoaji uliongezeka kwa aslimia 22% kutoka tani 23,000 hadi tani 29,000. Uwekezaji zaidi wa shilingi milioni 450 umepangiwa mwaka ujao kuongeza kiwango cha utoaji kimea katika kiwanda hicho hadi tani 34,00, ili kutosheleza mahitaji yanayoongezeka miongoni mwa idara za utengenezaji pombe za EABL na kuendelea kujitosheleza kwa mali ghafi.

Biashara ya UDVK imekuwa nzuri katika F07, ikikua katika faida na pia masoko. Tumepata manufaa ya kuunganisha utengenezaji mvinyo kali katika shughuli za EABL huko Ruaraka na kuwekeza katika mfumo mpya wa kisasa wa upakiaji katika kipindi kilichopita cha matumizi ya fedha. Faida ya UDV imekua kwa aslimia 98 katika kipindi cha mwaka uliopita.

Bidhaa zetu zinaendelea kufanya vyema katika soko la humu nchini na kupata ukuaji wa jumla wa 60%. Ukuaji huo ulitokana na uvumbuzi pamoja na uwekezaji katika bidhaa maarufu kama vile Richot, Smirnoff, Smirnoff Ice, Johnnie Walker, Baileys na VAT 69. Richot ilikuwa na uhamasishaji wa kitaifa wa wateja uliofahamika sana na kuifanya kujikita zaidi kwenye soko. Tulianzisha upya mvinyo wa VAT 69 katika soko na kuupa hadhi mpya, na kuwapa wateja wa pombe kali thamani nzuri kwa pesa zao. Mbinu yetu ya kupanua aina ya vinywaji vyetu kwa kuanzisha Smirnoff Black Ice imefanikiwa sana huku kiwango hicho kikidhihirisha ukuaji wa 21% katika F07.

Pombe kali za kipato cha chini kwenye soko zimekuwa na ukuaji wa kiwango cha juu na kushiriki kwetu katika kiwango hiki kupitia Kane Extra Golden kumekuwa hadithi ya ufanisi. Imetusaidia kupata wateja wengi zaidi kutumia pombe kali rasmi na pia kukabiliana na ushindani.

Tunatambua juhudi ambazo serikali imefanya katika kuifanya rasmi sekta hii kwa kuanzisha ushuru miongoni mwa nyingine. Bidhaa zetu zote sasa zina mhuri kama thibitisho kwamba zimelipiwa ushuru.

Kutokana na kukua kwa uchumi, UDVK sasa iko katika nafasi nzuri ya kutumia soko la humu nchini na pia masoko ya eneo hili.

Ujenzi wa kituo cha matibabu ya macho Arusha, Tanzania ambacho kimefadhiliwa na wakfu wa EABL.

Uganda

Uganda Breweries Limited ilikuwa na biashara nzuri kwa kipindi cha mwaka huo huku viwango vya pombe vikiongezeka kwa 22% na mvinyo kali kwa 26% na haswa kutokana na biashara ya Uganda Waragi na uzingatiaji wa soko la mvinyo kali.

Tulianza kukuza shayari nchini Uganda kwa kusajili wakulima 4,000 wa mashamba madogo madogo na shughuli zetu sasa zinajumuisha maeneo ya Kapachorwa na Bukwo mashariki mwa Uganda na eneo la Kabale kusini magharibi mwa nchi hiyo. Maeneo yote mawili yanafaa kwa ukuzaji shayiri.

Ukuzaji shayiri nchini Uganda hutekelezwa kupitia mashirika ya kijamii yanayohusisha wakulima 50 wa mashamba madogo madogo kila moja. Mashamba hayo ni ya kiasi cha kutoka nusu ekari hadi ekari tatu. Wakulima wamepewa mafunzo kuhusu uzalishaji shayiri na wafanyikazi wa East African Maltings - Uganda ili kutengeneza pombe ya Senator Lager, ambayo hutozwa ushuru wa chini.

Tanzania

Nchini Tanzania, umiliki wetu wa aslimia 20% ya hisa katika Tanzania Breweries umetufaidi na pombe yetu maarufu ya Tusker imekua na kudhibiti aslimia 20% ya soko. Tangu kuanzishwa kwa Malta Guinness kwenye mkebe ukuaji wa jumla umezidi matarajio. Wakfu wa EABL pia unaendelea kuwekeza kiasi kikubwa katika huduma za maji, elimu na afya nchini Tanzania.

Kuleta mabadiliko yenye manufaa

Kukuza unywaji wa Hekima

Kwa muda mrefu EABL imeamini kwamba unywaji pombe unaweza kuwa sehemu ya maisha na afya njema. Ijapokuwa tunakubali pia kwamba inapotumiwa kwa wingi, Pombe inaweza kusababisha matatizo makubwa ya afya na pia ki-jamii. Ukweli huu umetufanya kubuni kampeini mwafaka ya kuhimiza wateja wetu katika nchi tunakoendesha biashara yetu wanywe kwa uwajibikaji. Mwaka uliopita tulitumia shilingi milioni 125 kuhimiza wateja wetu wazingatie maadili mbali mbali ya hekima katika unywaji wao.Kuwasilisa ujumbe wetu tunatekeleza mipango kadha inayohusisha washikadau mbalimbali, ikiwa ni pamoja na:

Mafunzo kwa wahudumu wa Baa

EABL imeamua kuhusisha wahudumu wa Baa katika kuendeleza kampeini ya unywaji wa hekima. Mnamo miaka mitatu iliyopita tumewapa mafunzo wahudumu 3,500 wa baa na kuwafunza mbinu mwafaka za kuzuia watu walio na umri mdogo kunywa pombe na pia wateja waliolewa kupindukia. Mwaka ujao tuna mipango ya kuimarisha mpango huo ili kuhusisha wahudumu wengi zaidi wa Baa, bila shaka ikifahamika kwamba wao ndio wanawafahamu wanywaji wa pombe vyema zaidi.

'Unywaji wenye uwajibikaji ni muhimu kwa manufaa ya kila mmoja. EABL itakuwa mstari wa mbele kwa usambazaji habari za kuwezesha wateja kufanya maamuzi yafaayo.'

Mapambo ya biashara na kampeini za vyombo vya habari

Tulitayarisha mapambo na matangazo ya biashara na kueneza ujumbe kupitia kwa mabango, Magazeti, Majarida, Radioni na kwa njia ya Runinga chini ya kampeini zetu za "Kunywa kwa hekima, ishi kwa hekima'. Matangazo hayo yamelenga wateja wetu ambao binafsi wanahusika na tabia zao za unywaji. Pia tuliandaa warsha kwa wana-habari ili kuwapa ufahamu zaidi juu ya utumizi mbaya wa pombe na kusaidia kubadili jinsi maswala ya utumiaji mbaya wa pombe yanavyoangaziwa katika vyombo vya habari.

Kanuni za uuzaji

EABL imejitolea kuthibiti vilivyo shughuli zake katika sekta ya pombe, kwa kuweka viwango vya kimataifa na kuhakikisha kwamba bidhaa zetu zinatafutiwa masoko na kutangazwa kwa njia ifaayo. EABL imeanzisha na kutekeleza 'mfumo wa uuzaji wa Diageo' ambao huweka masharti ya uuzaji na kutangazwa kwa viburudisho vya pombe. Kwa mfano, mfumo huu unakataza matangazo au mapambo ya kibiashara yanayohusisha warembo wa chini ya umri wa miaka 25. Pia tunahakikisha kwamba Chupa za bidhaa zetu zina onyo la 'Sio ya kuuzwa kwa watu wa chini ya umri wa miaka 18'. Pia hatuuzi bidhaa zetu kupitia kwa vioski.

Sera ya pombe kwa wafanyikazi

Pia tumeratibu sera ya pombe kwa wafanyikazi wetu, inayohakikisha kwamba wafanyikazi wote wa EABL wanafahamu na kuelewa vyema mienendo ifaayo ya unywaji pombe. Sera hii inahusisha mafunzo kadha muhimu kama unywaji na uendeshaji gari, Pombe na mazingira ya kazi na shida za unywaji pombe. Wafanyikazi wote wa EABL wanahitajika kudhihirisha mfano mwema wa unywaji wa hekima.

Makala ya Kila Wiki juu ya unywaji wa hekima

Tuliwezesha kuchapishwa kwa ukurasa wa maswali na majibu na kumhusisha Daktari maarufu wa humu nchini katika makala

Waanzilishi wa Nabak nchini Kenya washerehekea ufanisi wa uzinduzi wake.

Waziri wa Habari na Mawasiliano Mheshimiwa Mutahi Kagwe azindua kitabu kiitwacho 'Drinking in Context'yaani kunywa kwa njia ifaayo, kilichopata msaada kutoka kwa EABL kuambatana na mpango wa Kunywa kwa Uwajibikaji.

Kuleta mabadiliko yenye manufaa



ya kila Ijumaa ya gazeti la Daily Nation. Kupitia makala haya wateja wana fursa ya kuuliza maswali kuhusu pombe.

Kuzuia watu wa umri mdogo kunywa pombe

Tuliandaa kongamano mwaka huu lililojumuisha wadau mbali mbali katika kujadili athari za pombe kwa watu wa umri mdogo. Kutokana na hali hiyo, EABL ilishirikiana na chama cha kitaifa cha maswala ya mvinyo na pombe katika uzinduzi wa kampeini ya 'WE ID' na kusaidia kukomesha unywaji wa watu wa umri mdogo.

Pia tunaendelea kushirikiana na wizara ya afya nchini Kenya na Uganda ili kutunga sera za kitaifa kuhusu pombe, ambazo zitasaidia viongozi wa sekta hii na watunzi wa sera kushughulikia matatizo kama lile la unywaji pombe wa watoto wenye umri mdogo.

Wajibu Wa Kijamii Wa Wakfu wa EABL

Kwa kipindi cha mwaka uliopita, wakfu wa Kampuni ya EABL umekua na kuimarisha zaidi maisha ya zaidi ya watu 250,000 katika kanda hii ya Afrika mashariki. Hapa ni baadhi ya vidokezi vya majukumu ya wakfu huu:

Ufugaji Samaki huko Nakasongola

Mradi uliozinduliwa hivi majuzi wa kufuga samaki wa shamba la Ekitangala huko Nakasongola, nchini Uganda, umeanza kuzaa matunda huku samaki wengi wakizalishwa kwenye vidimbwi.

Wakfu huo ulitoa mchango wa Ushs.22.5 milioni kusaidia kuchimba kisima kwenye shamba hilo. Kisima hicho sasa kinatoa maji kwa mabwawa sita ya shamba hilo na pia kwa matumizi ya nyumbani miongoni mwa jamii zilizo karibu.

Samaki wa shamba hili watakomaa hivi karibuni. Limetoa ajira kwa wafanyikazi 50 na pia hutumika kama kituo cha mafunzo kwa jamii. Shamba la samaki la Ekitangala pia hutoa huduma za afya kwa eneo la Katooge, mojawapo ya maeneo masikini zaidi nchini Uganda.

Maji kwa Uzima

Zaidi ya asilimia 60 ya visima vya kijamiia katika wilaya ya Kajiado nchini Kenya havitumiki kwa sasa kutokana na usimamizi mbaya wa jamii husika. Wilaya hiyo iliathiriwa vibaya na baa la njaa miaka ya 2004 na 2006 na watu wanaoishi katika

Jamii huko Kabale, Uganda yafunzwa kujenga matangi ya kuteka maji ya mvua.

Mkulima anavuna samaki kwenye mradi wa Maji ni Uhai huko Ekitaangala nchini Uganda.

ardhi ya makundi ya ufugaji wamepoteza idadi kubwa ya mifugo -tegemeo lao la pekee ki-uchumi.

Mradi wa maji kwa uzima wa wakfu huu kwa kushirikiana na shirika la AMREF-Kenya na jamii, ulijitahjidi kukarabati visima vinne katika eneo hilo. Mchango wa Wakfu huu wa zaidi ya shilingi milioni 5.7 za Kenya utanufaisha zaidi ya watu 5,000 na mifugo wao.

Wafanyikazi wa EABL, Wakiongozwa na mdhamini mkuu wa Wakfu wa EABL, Bw. James Karegi, walisaidia kuweka jiwe la msingi kwa mradi wa tangi jipya la maji ambalo litakuwa kituo kikuu cha maji kutoka visima vyote vinne.

Nchini Uganda, tumechangia miradi ya maji katika sehemu za Kabale na Kapchorwa. Kadhalika kituo cha kuvuna maji ya mvua kimezinduliwa huko Kabale. Mnamo mwaka ujao, tuna mipango ya kuwafikia raia wengi zaidi wa Uganda katika miradi yetu ya maji.

Mchango kwa Hospitali ya kimataifa ya Kampala

Wakfu huu uliwekeza katika Hospitali ya kimataifa ya Kampala katika ununuzi wa vitanda na matibabu ya wagonjwa. Udhamini huu wa shilingi milioni

Kueta mabadiliko [illegible]

Kundi la E-Green na shirika la Huduma kwa Wanyama Pori wakati wa shughuli ya upanzi wa miti

27.2 za Uganda utasaidia wagonjwa wasiobahatika ambao wanahitaji matibabu maalum lakini hawamudu gharama yake.

HIV/Aids

Kuongeza ufahamu kupitia sera ya pombe kwa wafanyikazi wetu kulituwezesha kutunukiwa heshima ya kongamano la wafanyibiashara wa Uganda dhidi ya janga la HIV/Aids. Sera ya kupambana na ukimwi katika matawi yetu itatoa matibabu ya maisha kwa wafanyikazi na jamaa zao.

Kiliniki ya Upasuaji macho huko Moshi

Wakfu huo umechangia ujenzi wa Kliniki ya matibabu ya macho kwenye taasisi ya Kikristo ya Kilimanjaro huko Moshi, Nchini Tanzania.

Kituo hiki cha wakfu wa EABL kitakuwa cha kipekee kinachoshughulikia visa vya upasuaji na shida nyingine za macho. Kituo hiki kitawanufaisha watu 10,000 katika maeneo ya Moshi na Arusha. Watu walio na shida za upofu au kuto-ona vizuri watapata usaidizi wa kimatibabu na pia kufanyiwa upasuaji, hivyo kuwezesha wengi wao kurejea kazini na kuendelea kutumikia jamaa zao.

Ujenzi wa kituo hicho umenza na huenda ukakamilika mwishoni mwa mwaka huu wa 2007. Mara tu kikianza kufanya kazi, kuna uwezekano wa kituo hiki kutembelewa na zaidi ya watu 50 kwa siku.

E-Green

E-Green, ambao ni mradi wa mazingira unaoendeshwa na wafanyikazi wa kampuni ya EABL, ulipanda zaidi ya miti 2000 katika hifadhi ya msitu wa Ngong mjini Nairobi ambao uliharibiwa na jamii zinazoishi karibu.

Wakfu huo pia ulitoa mchango wa shilingi 200,000 kwa hazina ya hifadhi ya msitu wa Ngong, ambalo ni kundi linalotetea kupandwa upya kwa miti katika hifadhi hiyo ya msitu wa Ngong.

Msitu huo ambao uko umbali wa takriban kilomita sita kutoka jijini Nairobi umekumbwa na tatizo la wakataji miti,jamii iliyo karibu na wanyakuzi wa ardhi.

Mradi wa E-Green, pia umesaidia kupanda miti katika maeneo ya Mau Narok na Gatanga nchini Kenya, Msitu wa Kkoba, Namanve na katika kiwanda cha kampuni ya Uganda Breweries mjini Kampala. Mradi wa E-green una lengo la kuhimiza uhifadhi wa mazingira kwa kuwahamasisha na kuwatia moyo wafanyikazi na jamii kwa ujumla.

Misaada ya masomo mwaka wa 2007

Wahitimu 14 werevu wa shule za upili na ambao wanatoka jamaa masikini nchini Kenya, Uganda na Tanzania wametunikiwa misaada ya masomo ya wakfu wa EABL ili kuendelea na masomo ya shahada katika vyuo vikuu mbali mbali vya Afrika mashariki. Wanafunzi hao walichaguliwa kati ya 7,000 waliotuma maombi kutoka eneo zima la Afrika mashariki. Misaada hiyo ya masomo ni ya jumla ya shilingi milioni 19 za Kenya.

Kila msaada wa masomo unajumuisha ada ya karo na gharama ya malazi kwa muda wa masomo wa miaka minne. Wanafunzi hao kadhalika watapokea marupurupu ya kujikimu wakati wa kipindi cha masomo yao na pia nafasi za ushauri na mafunzo ya kikazi katika matawi ya kampuni hii ya EABL.Huu ni mwaka wa saba kwa misaada ya masomo ya EABL kutolewa, huku wanafunzi 70 wakiwa wamenufaika kwa gharama ya shilingi milioni 90 za Kenya.

Huduma kwa kina mama wajawazito

Kituo cha afya cha Kirwara katika mkoa wa kati nchini Kenya kilipokea mtambo wa kisasa wenye thamani ya zaidi ya shilingi milioni 1 kutoka kwa wakfu huu ili kusaidia katika kuwachunguza kima mama wajawazito. Kwa kutoa mtambo huo, Wakfu huo utasaidia kina mama wajawazito ambao awali walihitajika kusafiri zaidi ya kilomita 30 ili kufanyiwa uchunguzi.

EAST AFRICAN BREWERIES LIMITED

Tusker Lager yaelekea Ncha ya Kaskazini

Watalii waliozuru Kenya ambao walipendelea sana bia maarufu ya Kenya ya Tusker Larger walipendezwa sana na ladha yake hivi kwamba waliamua kwenda nayo kwenye safari maalumu katika Ncha ya Kaskazini mwa dunia.

Pete Goss mzungumzaji wa masuala ya uhamasishaji na baharia alifikiria lingekuwa wazo ambalo halijawahi kufanywa kwenda na Tusker na Bendera ya Tusker hadi Ncha hiyo ya dunia yenye sumaku. Hata hivyo alisema pombe hiyo ilipaswa kutumiwa muda mfupi kabla ya Kafika mahala hapo kwani ingesalia imeganda kwa miaka mingi lakini bendera ilifanikiwa kukamilisha safari hiyo na kufika Ncha ya Kaskazini zaidi mwa dunia.

"Nilisikia kwa mara ya Kwanza juu ya Tusker wakati wa ziara yangu nchini Kenya na nikaipenda mara tu nilipokunywa moja baridi baada ya siku yenye joto - ningali ninaona mtonesho wake na kuonja ladha yake sasa", Goss alisema.

Goss ambaye ni mmoja wa watu wachache waliosafiri ulimwegu mzima mara mbili kwa mashua alisema alivutiwa na Ncha hiyo baada ya kusoma kuihusu katika vitabu vilivyoandikwa na wapelelezi maarufu na kuamua kujionea mwenyewe. Hii ilikuwa ziara yake ya nne.

"Niliipenda mara ya Kwanza nilipoiona na sasa ninaendesha biashara ndogo ambapo sisi huwafunza wanagenzi kisha huwapeleka kusimama juu ya ulimwengu, jambo ambalo ni la kustaajabisha kweli," alisema.

Ni katika ziara yake ya nne ambapo alibeba chupa ya Tusker. "Nilibeba moja tu kwani hali ilikuwa ya baridi kali katika Ncha ya Kaskazini. Ilibidi kuitunza ili isigande kutokana na baridi."

Kwa maoni yake, Tusker Lager ni pombe ya kiwango cha kimataifa. "Nimeonja pombe nyingi kote ulimwenguni na Tusker ina mvuto unaostahili.Kitu kingine ambacho nakipenda, kama mpenda mahaba kiasi, ni umaarufu wa bidhaa yenyewe na historia. Unawezaji kukosa kuguswa na hadithi, nchi na urithi kama huo? Daima nitakuwa balozi."

Sio wengi wanaoweza kudai kuwa na tajriba ya safari kama hiyo na sasa tuna Tusker Lager ya hapa kwetu Kenya kuongezea kwa wachache hao.

EAST AFRICAN BREWERIES LIMITED

Corporate Information

FINANCIAL CALENDAR
For the year ended 30 June 2007

RESULTS
Half Year Results announced on 23 February 2007
Full Year Results announced on 31 August 2007

Annual Report
Issued on 5 October 2007
85th Annual General Meeting:
1 November 2007

DIVIDENDS
Interim
Announced on 23 February 2007
Paid on 12 April 2007

Final
To be declared on 1 November 2007
Payable on or about 5 November 2007

Register
Closing date: 12 October 2007

BOARD OF DIRECTORS & ADMINSTRATION
Group Chairman
J G Kiereini EGH, EBS, SS
Group Deputy Chairman
N Blazquez *
Group Managing Director
G K Mahinda
Group Commercial Director
C Caldwell*

Non-Executive Directors
R Kemoli
W S Kalema (Or) **
E Mwaniki
W Mugane (Ms)
B A Savage ***
A M Ndegwa

*British **Ugandan ***Nigerian

Group Company Secretary
A Murgor (Mrs)
(Appointed on 30 August 2007)

BOARD COMMITTEES
Board Audit & Risk Management Committee
R Kemoli, Chairman
N Blazquez (Dr)
B Savage
A M Ndegwa

Board Remuneration Committee
N Blazquez (Dr), Chairman
W Kalema (Dr)
E Mwaniki

Board Corporate Governance Committee
W Mugane (Ms), Chairperson
R Kemoli
E Mwaniki
W Kiboro

Board Nominations Committee
N Blazquez, Chairman
W Kalema (Dr)
R Kemoli
W Mugane (Ms)

REGISTERED OFFICE & PRINCIPAL PLACE OF BUSINESS
Corporate Centre, Ruaraka
Off Thika Road
P O Box 30161 - 00100
Nairobi
Telephone: 864000
Fax: 8563054/8561090
Email: info@eabl.com

REGISTRAR
Custody & Registrar Services Limited
6th Floor, Bruce House
Standard Street
P O Box 30120 - 00100
Nairobi

AUDITORS
KPMG Kenya
Lonrho House, 16th Floor
Standard Street
P O Box 40612 - 00100
Nairobi

BANKERS
Standard Chartered Bank Kenya Limited
Kenyatta Avenue Branch
P O Box 30001 - 00100
Nairobi

Commercial Bank of Africa Limited
CBA Building
Wabera/Standard Street
P O Box 30437 - 00100
Nairobi

Barclays Bank of Kenya Limited
Barclays Plaza
Loita Street
P O Box 30120 - 00100
Nairobi

Citibank NA
Citibank House, Upper Hill Road
P O Box 30711 - 00100
Nairobi

ADVOCATES
Kaplan & Stratton
Williamson House, 4th Ngong Avenue
P O Box 40111 - 00100
Nairobi

EAST AFRICAN BREWERIES LIMITED

Notice of Annual General Meeting

NOTICE IS HEREBY GIVEN that the EIGHTY FIFTH ANNUAL GENERAL MEETING of East African Breweries Limited will be held at Safari Park Hotel, Ruaraka, Nairobi on 1 November 2007 at 11 a.m. for the following purposes:

1. FINANCIAL STATEMENTS

a) to receive and adopt the audited financial statements for the year ended 30 June 2007 together with the report of the Directors and the Auditors' report thereon **(Resolution 1);**

b) to confirm the interim dividend of KShs 2.15 and declare a final dividend of KShs 5.55 per ordinary share payable on or about 5 November 2007 to members on the Register at the close of business on 12 October 2007 **(Resolution 2);**

c) to consider and if approved, adopt the following resolutions which will be proposed as ordinary resolutions:

i) "**THAT** pursuant to Article 15B of the Company's Articles of Association, it is desirable to capitalize the sum of KShs 263,591,452 being part of the sum standing to the credit of the share premium reserve and that accordingly such sum be set free for distribution amongst the holders of ordinary shares in the capital of the Company on the register of the members on 12 October 2007, on condition that the same not be paid in cash but be applied in paying up in full at par 131,795,726 ordinary shares of KShs. 2 each in the capital of the Company, and that such 131,795,726 shares credited as fully paid up be accordingly allotted to such persons respectively in the proportion of one (1) of such shares for every five (5) of the ordinary shares then held by such persons respectively (fractions of a share to be disregarded) and that the shares so distributed shall rank pari passu with the existing issued ordinary shares and shall be treated for all purposes as an increase of the nominal amount of the capital of the Company held by each such shareholder and not as income and the Directors be and are hereby authorized and directed to attend to all matters required to give effect to this resolution.". The bonus issue is subject to the approval of the Capital Markets Authority being obtained and to the Nairobi Stock Exchange approving the listing of the new ordinary shares of the company. **(Resolution 3);**

ii) "**THAT** in pursuance of Article 160 of the company's Articles of Association should any of the said bonus shares be not issued by reason of fractions of a share being disregarded, the Directors may allot and issue the same to such persons and upon such terms and conditions as they may deem fit." **(Resolution 4);**

2. DIRECTORS

a) Elections

i) to re-elect Mr. Babatunde Savage who retires by rotation under Article 109 and being eligible, offers himself for re-election as a director of the company **(Resolution 5);**

ii) to re-elect Mr. Andrew Ndegwa who retires by rotation under Article 109 and, being eligible, offers himself for re-election as a director of the company **(Resolution 6);**

iii) to re-elect Mr. Wilfred Kiboro who retires by rotation under Article 109 and, being eligible, offers himself for re-election as a director of the company **(Resolution 7).**

b) Remuneration

To note that the Directors are not seeking any increase in their remuneration, which, accordingly, remains as, stated in the financial statements.

3. AUDITORS

To appoint KPMG Kenya, the company's Auditors for the period ending with the next annual general meeting of the company and to authorise the directors to determine their remuneration **(Resolution 8);**

4. To transact any other business that may legally be transacted at the meeting.

By Order of the Board,

A Murgor (Mrs)
Secretary
31 August 2007

A member entitled to attend and vote at the meeting is entitled to appoint one or more proxies to attend and vote on his behalf. A proxy need not be a member.

A tear-out form of Proxy is given on page 75 for use by members who do not propose to be present at the meeting. A Form of Proxy must be returned to the Company Secretary by no later than 11.00 am on Tuesday 30 October 2007, being not less than 48 hours before the time appointed for the meeting.

Pursuant to Article 107 of the company's Articles of Association, any member may by notice duly signed by him and delivered to the Secretary of the company not less than seven days and not more than twenty-eight days before the day appointed for this meeting propose any other person for election to the Board. Such notice must be accompanied by a notice signed by the person proposed, indicating his willingness to be elected.

EAST AFRICAN BREWERIES LIMITED

ILANI INATOLEWA HAPA KWAMBA MKUTANO MKUU WA MWAKA WA THEMANINI NA TANO WA KAMPUNI YA East African Breweries Limited utafanyika katika Safari Park Hotel, Ruaraka, Nairobi, tarehe mosi Novemba, 2007 saa tano asubuhi kwa shughuli zifuatazo:

1. TAARIFA ZA KIFEDHA

a) kupokea na kuidhinisha taarifa za ukaguzi wa fedha kwa kipindi cha hadi terehe 30 Juni mwaka 2007 pamoja na ripoti za wakurugenzi na wakaguzi wa fedha juu ya ukaguzi huo **(Azimio 1)**;

b) kuidhinisha mgao wa muda wa faida wa Kshs 2.15 na kutangaza malipo ya mwisho ya mgao wa faida ya KShs5.55 Kwa kila hisa ya kawaida ambayo yatatolewa tarehe 5 Novemba, 2007 kwa wanachama walisajiliwa kufikia wakati wa kufunga biashara tarehe 12 Octoba, 2007 **(Azimio 2)**;

c) Kutafakari na ikikubaliwa kuidhinisha maazimio yafuatayo ambayo yatapendekezwa kama maazimio ya kawaida:

